


HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE

[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Temeke]

Simu: +255 22-292832
Fax: +255 22-2928137
Barua pepe: temeke@temekemc.go.tz
Tovuti: <http://www.temekemc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi
92 Barabara ya Mandele/Taifa
S.L.P: 46343,
15833 - DAR ES SALAAM,

Kumb Na. TMC/MD/A.5/

Tarehe: 26/09/2017

TANGAZO

NAFASI YA KAZI (INARUDIWA)

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke anawatangazia Wananchi/Watanzania wote wenye sifa zinazotakiwa kuomba kujaza nafasi ifuatayo:-

1. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 1)

➤ SIFA/ELIMU/UJUZI

- Elimu ya kidato cha **IV**, na leseni ya daraja la E au C. 1 ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila ya kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (basic driving course). Yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.

KAZI NA MAJUKUMU

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kufanya matengenezo madogo madogo kwenye safari za kikazi.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- kufanya usafi wa gari na
- kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelekezwa na msimamizi wake.

NGAZI YA MSHAHARA

Ataanza mshahara **TGOS A (1)** kwa mujibu wa viwango vya Serikalini.

UMRI

Waombaji wote wanatakiwa wawe na umri usiopungua miaka **18** na usiozidi miaka **45**.

MAELEZO YA JUMLA

Maombi yote yawasilishwe yakiwa yameambatanishiwa na CV pamoja na nakala za vyeti vya kuhitimu elimu na mafunzo (vyeti vinavyoonyesha kiwango cha kufaulu na sio 'leaving certificate')

